***BISMILLAHIR-RAHMANIR-RAHIIM***
LUQMAN ISLAMIC SEMINARY
P.O.BOX 33820, DAR ES SALAAM MOB: 0717 122 415, 0692 314 873, 0713 513 041
Email: luqmanislamic1921@gmail.com //////////////////////... CENTRE NO. 1921
*Education is Light*

**JARIBIO LA MWEZI**
**KIDATO CHA KWANZA**
**HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

**Muda: SAA 2:30** **MACHI 2025**

**Maelekezo**
1. Mtihani huu umekusanya maswali **10** katika sehemu A, B and C.
2. Jibu mwaswali yote katika sehemu zote.
3. Simu ya mkononi hairuhusiwi na vitu visivyohusika katika chumba cha mtihani .
4. Andika jina katika kila ukurasa wa karatasi yako ya kujibia.

| KWA MSAHIHISHAJI PEKEE | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **MAKSI** | **SAHIHI** |
| **1.** | | |
| **2.** | | |
| **3.** | | |
| **4.** | | |
| **5.** | | |
| **6.** | | |
| **7.** | | |
| **8.** | | |
| **9.** | | |
| **10.** | | |
| **JUMLA** | | |

i.) Mwalimu wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili alipoingia darasani kwa mara ya kwanza aliwaambia wanafunzi wake wapendwa kuwa somo hili limejikita katika dhana kuu mbili nazo ni:

A. Mabadiliko ya Tanzania na Maadili yake

B. Historia ya Tanzania na Mabadiliko yake

C. Historia ya Tanzania na Maadili

D. Maadili na Historia ya Dunia

ii.) Kumekuwa na uhusiano mkubwa kati ya somo la Historia ya Tanzania na masomo mengine, ukiacha masomo mengine, somo hili lina husiana na somo la Jiografia kwa kuwa:

A. Somo la Jiografia linajihusisha kuelewa aina za vyakula walivyotumia babu zetu

B. Somo la Jiografia linajihusisha kutoa burudani kwa watu Tanzania

C. Somo la Jiografia linajihusisha kujua lugha mbalimbali walizotumia watu

D. Somo la Jiografia linajihusisha mazingira ambayo historia imetokea

iii.) Ili Taifa lolote liendelee watu wake hawana budi kushikamana na maadili, hivyo maadili yaweza kutafsiriwa kama ni:

A. Miongozo inayotawala tabia na matendo ya watu

B. Matendo yanayotawaliwa na watu mbalimbali

C. Miongozo inayotawala viongozi mbalimbali

D. Mambo muhimu yanayotawala historia ya watu

iv.) Wazee wa jamii zilizopita walijitahidi kuwafunza vijana chipukizi katika suala la kufuata maadili ya jamii zao, mafunzo hayo yalitolewa kwa kuzingatia:

A. Uchumi na siasa za jamii husika

B. Mila na desturi za jamii husika

C. Uelewa na ufahamu wa wanajamii

D. Maamuzi ya viongozi wa dola zilizokuwepo

v.) Jamii ya Wabantu ni miongoni mwa jamii za kale zilizosambaa maeneo mengi barani Afrika, jamii hii asili yake ni kutoka maeneo ya:

A. Kusini mwa Bara la Afrika

B. Kaskazini mwa Bara la Afrika

C. Magharibi mwa Bara la Afrika

D. Mashariki mwa Bara la Afrika

vi.) Katika chemsha bongo alyoitoa mwalimu darasani kwa kuwapa wanafunzi vijikaratasi vilivyoandikwa hifadhi za taifa. Kipenseli aliibuka kidedea kwa kuchagua hifadhi iliyosheheni michoro ya kale kama mwalimu alivyowataka kufanya. Unadhani ni hifadhi gani hiyo?

A. Ngome Kongwe

B. Kondoa Irangi

C. Jumba la maajabu

D. Ngorongoro

vii.) Nazminho ni Mtanzania anayefanya kazi katika Umoja wa Mataifa shirika linalohusika na utambuzi wa Urithi wa Asili kimataifa, hivyo ametoa mchango mkubwa katika kutambulika Urithi unaopatikana Tanzania. Kwa kutumia maarifa yako unadhani Nazminho anafanya kazi shirika gani kati ya haya:

A. DAWSCO

B. TANESCO

C. UNESCO

D. LEGCO

viii.) Tunu ni jambo ambalo watu hupewa bila kuomba, Tanzania imebarikiwa tunu mbalimbali kama zifuatazo isipokuwa:

A. Umoja na Usawa

B. Uhuru na Utu

C. Uadilifu na Uzalendo

D. Uvivu na Ukatili

ix.) Wazee ambao ni watangulizi wetu katika Taifa la Tanzania wametuachia urithi ambao mpaka leo tunajivunia nao. Moja katika vifungu vifuatavyo vinabainisha aina za urithi huo.

A. Urithi unaoshikika, unaomilikika na urithi usiomilikika

B. Urithi usioshikika, unaoshikika na urithi wa asili

C. Urithi usioshikika, unaomilikika na urithi wa asili

D. Urithi unaoshikika, usiomilikika na urithi wa asili

x.) Nchi yetu ya Tanzania imeongozwa na Maraisi mbalimbali, wafuatao wametawala kwa kuongozana.

A. Nyerere kisha Mkapa

B. Mwinyi kisha Kikwete

C. Mkapa kisha Kikwete

D. Magufuli kisha Kikwete

2. Oanisha Makabila ambayo ni asili ya Tanzania yaliyo katika Kundi A na maelezo ya makabila hayo yaliyo Kundi B

| **KUNDI A** | **KUNDI B** |
|---|---|
| i.) Wabantu<br>ii.) Wanilo<br>iii.) Wakichembe<br>iv.) Wangoni<br>v.) Wakushito | A.) Jamii ambayo ni wazawa halisi wa Tanzania<br>B.) Jamii ya waliohama kutoka Kusini mwa Bara la Afrika<br>C.) Jamii ya waliohama kutoka eneo lililopo kati ya nchi ya Naijeria na Kameruni<br>D.) Jamii ya waliohama kutoka kwenye kona ya Afrika maeneo ya Somalia na Ethiopia.<br>E.) Jamii ya asili ya Tanzania iliyohama kutoka bara la Asia mpaka Afrika<br>F.) Jamii ya asili ya Tanzania iliyohama kutoka bara la Amerika mpaka Afrika<br>G.) Jamii ya asili ya Tanzania iliyohamia kutoka Sudani |

**SEHEMU B (Alama 70)**

**Jibu maswali yote kutoka sehemu hii**

3. Serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania haikuanzisha ufundishwaji wa somo hili la Historia ya Tanzania na Maadili kwa kukurupuka, bali ilizingatia faida zinazopatikana. Kwa kifupi fafanua faida tano miongoni mwa hizo.

..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
......................

4. Tanzania imepitia hatua mbalimbali na kugubikwa na matukio mengi mpaka kufikia hapa tulipo, ukiwa kama mwanahistoria elezea matukio matano unayoyakumbuka.

..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................
......................

6. Maadili ni nyenzo muhimu katika kujenga maendeleo ya taifa lolote duniani, hivyo kwa Taifa la Tanzania umuhimu wa maadili unaweza kutazamwa katika mambo kadhaa, fafanua matano tu.

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
.....................

7. Somo la Historia ya Tanzania na Maadili siyo somo lililopwekeka peke bali lina uhusiano na masomo mengine. Tumia weledi ulioupata kuelezea uhusiano wake na masomo yafuatayo:

i. Hisabati
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
....ii. Kiswahili na kiingereza
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
....

iii. Chakula na Lishe

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
....iv. Sanaa na Michezo

..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
....v. Kilimo
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
..........................................................................................................................................
......

8. Mtoto mwenye tabia njema hupendwa na kila mtu, kwa kulijua hilo watangulizi wetu walijidhatiti vilivyo kuhakikisha wanapandikiza tabia njema kwa vijana chipukizi. Elezea mambo matano ambayo yanayosisitizwa katika kujenga tabia njema.

.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................

9. Kwa kutoa mifano kutoka jamii unayoishi, bainisha changamoto wanazopitia wazazi na watu wazima katika kujenga na kukuza maadili ya vijana kisha pendekeza jinsi ya kuzitatua changamoto hizo.

Changamoto
i.)..................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
...ii.)..............................................................................................................................
.....................................................................................................................................
......iii.)...........................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
...........

Mapendekezo

i.)..................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....ii.)............................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
..........

**SEHEMU C (Alama 15)**

**Jibu swali la 10 katika sehemu hii**

10. Bwana Greenhouse ni Mtalii kutoka Norway ambaye amevutika kuja Tanzania baada ya kuangalia filamu ya **’’Royal Tour’’** inayoeleza turathi za Tanzania zikiwemo hifadhi za Taifa. Ukiwa kama muongoza watalii, kwa kutumia Insha muelezee Bwana Greenhouse kuhusu hifadhi tano ambazo ungeweza kumtembeza.

..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................
..............................................................................................................................................
.............